# Fursa ukuaji sayansi

**Na Elizabeth Zaya**

WANASAYANSI chipukizi (YST), zaidi ya 200 kutoka katika shule mbalimbali nchini, wanatarajia kushiriki katika maonyesho ya kazi za sayansi Agosti mosi, mwaka huu jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam juzi, mwanzilishi mwenza wa YST, DK. Gosbert Kamugisha, alisema lengo la maonyesho hayo ni kuwapa fursa wanafunzi kutafiti na kuonyesha uwezo wa sayansi katika kutatua matatizo ya kijamii na kiuchumi yanayoikabili nchi.

Alisema wanasayansi chipukizi watakaofanikiwa kufanya ugunduzi mzuri watazawadiwa pesa taslimu, medali, vikombe na uimarishaji wa maktaba za shule zao.

Watakaofanya vizuri zaidi katika ugunduzi huo na kushika nafasi za juu, alisema mwanzilishi mwenza huyo, watapata udhamini wa masomo ya chuo kikuu ili kuwawezesha kusoma masomo ya sayansi na teknolojia katika ngazi hiyo.

"Wanasayansi chipukizi watakaoshiriki onyesho la YST mwaka huu kwa sasa wanaendelea kutengeneza kazi na miradi yao katika nyanja mbalimbali za kisayansi ikiwamo kemia, fizikia, hesabu, biolojia, ekolojia, sayansi ya jamii na tekonolojia," alisema Dk. Kamugisha.

"Kazi za miradi mingi zimejikita kutafuta suluhisho kuhusu matatizo katika sekta ya afya, kilimo, usalama wa chakula, mawasiliano na usafirishaji, nishati, elimu, mazingira na mabadiliko ya tabia nchi."

Dk. Kamugisha alisema wanafunzi watakaochaguliwa mbali na kupewa zawadi, pia wao pamoja na shule zao watapewa mafunzo kutoka kwa washauri wa sayansi kuhusu namna ya kutengeneza kazi zao za kisayansi.